

»Kugeuza maganda ya mpunga kuwa mbolea ya bei nafuu – Sehemu ya 1«

Athari za mabadiliko ya hali ya hewa nchini Kenya ni tofauti katika mikoa tofauti. Kila mkoa unakabiliwa na changamoto tofauti na uhaba wa maji, uhaba wa chakula na uchafuzi wa mazingira.

Uzalishaji wa mkaa una madhara mengi kama vile uharibifu wa mazingira kupitia ukataji miti. Ukataji miti ni kuondolewa kwa miti na misitu. Ukataji miti huchangia utoaji wa gesi ya hatari. Tani 15 za pumba za mpunga huzalishwa, na ama kuchomwa au kutupwa, jambo ambalo huathiri mazingira. Maganda ya mpunga huongeza uzalishaji maradufu yanapotumiwa kama mbolea shambani.

Uzalishaji mkaa kutoka kwa mabaki ya mazao (Biochar)

Biochar ni mkaa kutoka kwa taka za mazao. Kusanya maganda na makapi ya mazao kutoka kwa wakulima na uweke kwenye tanuru huku ukiyachoma kwa joto la juu ya angalau digrii 300. Baada ya masaa 2 utapata vichepechepe.

Pakia nyenzo kama vile maranda ya mbao kwenye tanuru na uzi ke tanuru na maganda ya mchele nje. Mara baada ya kubadilika kutoka njano hadi nyeusi basi ni tayari kuondolewa.

Saga pumba hizo nyeusi na ongeza virutubisho na uvichanganye vizuri, kisha uvifungashe.

Viwango vyatengenezwa katika uzalishaji

wa mbolea ya kikaboni

Udhibiti wa ubora ni muhimu katika suala la mbolea. Hakikisha unapata angalau 95% ya kaboni na kiwango cha unyevu kinapaswa kuwa chini ya 20%.

Halijoto linaweza kutofautiana kulingana na pH udongo.

Hakikisha kwamba unapofungasha, kiasi cha nyenzo zimechanganywa kwa uwiano sahihi.